# سؤال وجواب

# في

# أحكام الصيام

# SWALI NA JAWABU

# KUHUSU

# HUKUMU ZA SAUMU

**Mtunzi:**

**Sheikh Muhammad Bin Swaleh Al-Uthaymin**

**Tarjama:**

**Abu Halima Arafat Bin Mahmoud**

**Namba moja (1)**

## [NIA (KUNUWIA)]

**Swali:** Je, kunuwia siku ya kwanza katika mwezi wa Ramadhani kunatosheleza kuwa ndio Nia ya mwezi mzima?

**Jawabu:** Nia ya siku ya kwanza ya Ramadhani inatosheleza, wala si mwenye kuhitajia kuifanya upya Nia yake kila siku. Isipokuwa ikipatikana sababu ambayo ameruhusiwa yeye kula mchana (wa Ramadhani) atakula, na akitaka kuendelea tena na saumu atanuwia upya.

## [KUJIZUIA]

**Swali:** Ni ipi hukumu ya kula au kunywa wakati wa adhana ya alfajri au baada yake kidogo, hasa atakapokuwa mtu hakujua wakati wa kuchomoza alfajri?

**Jibu:** Mazingatio ni kuchomoza kwa alfajri, endapo muadhini ni muaminifu na anajulikana kwamba hatoi adhana isipokuwa ikichomoza alfajri ya kweli, basi atakapoadhini na mtu akasikia adhana yake ni wajibu wake kujizuia na kula au kunywa.

**Swali:** Pindi mtu akila daku akidhani kwamba bado ni usiku, kisha ikambainikia yeye kwamba alfajri tayari imechomoza, ni ipi hukumu ya funga ya siku hiyo?

**Jawabu:** Funga yake ni sahihi.

**Swali:** Tunaona baadhi ya kalenda katika mwezi wa Ramadhani kuna sehemu imeandikwa kujizuia (kula na kunywa) kiasi cha dakika kumi au robo saa kabla ya swala ya alfajri. Je hili lina dalili yoyote katika mafunzo ya Mtume ﷺ au ni bidaa?

**Jawabu:** Jambo hili ni miongoni mwa bidaa, wala halina ushahidi wowote katika sunna za Mtume ﷺ , bali sunna imekuja kuelezea kinyume chake, kwa sababu Allaah

anasema: **"Na kuleni na kunyweni mpaka ubainike kwenu weupe wa alfajiri kutoka katika weusi wa usiku. Kisha timizeni saumu mpaka usiku".** **[Al-baqara/187].** Na Mtume ﷺ amesema: **"Hakika Bilal anaadhini wakati wa usiku, basi kuleni na kunyweni mpaka msikie adhana ya Ibn Ummi Maktum, kwa sababu yeye hatoi adhana mpaka ichomoze alfajri".** **Kitabu: [Bukhari (1918) na Muslim (1092)].**

## [VITENGUZI VYA SAUMU/FUNGA]

**Swali:** Ni vitu gani vinatengua saumu/funga ya mtu?
**Jawabu:** Vitenguzi vya saumu vilivyotajwa ndani ya Qur'an ni vitatu: **kula, kunywa na jimai (tendo la ndoa)**.

Ama kula na kunywa ni sawa iwe ni kitu cha halali au haramu, au chenye manufaa au madhara, au kisicho na manufaa wala madhara yoyote, na ni sawa kilikuwa kichache au kingi, ndio maana kuvuta sigara kunatengua funga yako (na utazingatiwa hujafunga siku hiyo). Na kuhusu jimai (tendo la ndoa), nalo ndio kitenguzi kikubwa zaidi, kwa sababu ya kuwajibishwa ndani yake kutoa kafara, ambayo ni kuacha huru mtumwa, akishindwa ni kufunga miezi miwili mfufulizo, na akishindwa atalisha maskini sitini.

- **Kitenguzi cha nne:** Kujitoa manii/kujichua (sawa iwe kwa njia ya haramu kama vile kutumia mkono au kuangalia, n.k), au (njia ya ya halali kama vile kuchezacheza na mkeo mpaka yakatoka manii), lakini hakuna ndani yake kutoa kafara, kwa sababu kafara ni kwa kufanya tendo la ndoa. (na kama manii yakitoka yenyewe kwa sababu ya maradhi n.k funga yako ni sahihi),
- **Kitenguzi cha tano:** Kuchoma sindano ambazo hutumika badala ya chakula au kinywaji (mfano: sindano za vitamin 'c' n.k), tafauti na sindano zisizotumika kwa ajili hiyo, hizo

hazitengui funga ya mtu, hata kama sindano hiyo ilidunga mshipa au msuli, kwa sababu haijakaa nafasi ya chakula wala kunywa.

- **Kitenguzi cha sita:** Kujitapisha, na kama atazidiwa akashindwa kujizuia, basi hakuna chochote juu yake (funga yake ni sahihi).
- **Kitenguzi cha saba:** Kutoka kwa damu ya hedhi au nifasi, ikimtoka mwanamke damu ya hedhi au nifasi, funga yake itakuwa imebatilika, hata kama zimebaki dakika chache kabla ya kuzama jua, na kama itamtoka baada tu ya kuzama jua, basi funga yake ni sahihi.
- **Kitenguzi cha nane:** Kutoa damu kwa kufanya Hijama (kuumika/kupiga chuku), kwa hadithi ya Mtume ﷺ : **"Amefungua mwenye kufanya Hijama na mwenye kufanyiwa". Kitabu: [Al-irwaa (931)].** Ama kufungua kwa mwenye kufanya hijama ni pale atakapokuwa anatumia njia ya kuvuta damu kwa kinywa chake (njia ilivyokuwa ikitumika zamani), kwa sababu inahofiwa huenda alivuta damu ikapitiliza kwenye koo yake (matokeo yake akafungua). Lakini ikitumika njia za kisasa kiasi ambacho anatumia mikono tu bila kuvuta kwa mdomo wake, wakati huo itabatilika funga ya mwenye kufanyiwa pasi na mwenye kufanya. (pamoja ipo kauli kwamba hadithi hii imefutwa na hadithi nyingine).

**Ikiwa yamepatikana mambo haya (kula, kunywa, kufanya jimai) katika mchana wa Ramadhani kwa mtu ambaye ni wajibu juu yake kufunga,** basi yatapatikana kwake mambo manne:
(1) Atapata dhambi. (2) funga yake itabatilika. (3) itamlazimu kujizuia (bila kula) mchana wa siku hiyo mpaka jioni. (4) ni wajibu juu yake kuilipa siku hiyo.

Na kama alifanya jimai (tendo la ndoa), litaongeza kwake jambo la tano, ambalo ni kutoa kafara. Lakini ni wajibu

kufahamu kwamba vitu hivyo vyote vitazingatiwa kuwa vimebatilisha funga ya mtu kwa masharti matatu:

(1) elimu/kujua. (2) kukumbuka. (3) kufanya kwa hiyari bila kulazimishwa/kutenzwa nguvu.

**Sharti la kwanza ni elimu:** Endapo mtu atafanya hayo (kula, kunywa na jimai) katika mchana wa Ramadhani hali ya kuwa ni mjinga (hajui kwamba haifai), basi funga yake ni sahihi, ni sawa **hakujua wakati:** kama vile aliyekula baada ya kuchomoza alfajri akidhania bado ni usiku, au **hakujua hukumu:** kwamba Haifa kufanya Hijama ukiwa umefunga au kwamba Hijama inabatilisha funga.

**Sharti la pili ni kukumbuka:** wakati anakula, kunywa au kufanya jimai awe anakumbuka, lakini akifanya hayo kwa kusahau kwamba yeye amefunga, funga yake ni sahihi.

**Sharti la tatu hiyari:** lau mwenye kufunga alifanya moja ya mambo hayo bila ya hiyari yake, basi funga yake ni sahihi.

## Hukumu ya kula mchana wa Ramadhani bila sababu za kisheria

**Swali:** Ikiwa nimekula katika mchana wa Ramadhani (makusudi) bila sababu za kisheria, je nifunge siku moja kwa ajili ya kulipa siku hiyo au nifunge miezi miwili?

**Jawabu:** ikiwa amekula na wala hakufanya jimai (tendo la ndoa), basi itamlazimu yeye kutubia kwa Allaah (kwa dhambi hiyo) na pia kuilipa siku hiyo.

## Kufanya jimai (tendo la ndoa) mchana wa Ramadhani

**Swali:** Ni ipi hukumu ya mtu aliyefanya jimai na mkewe katika mchana wa Ramadhani bila kutokwa na manii, (tupu

ya mwanamme imeingia ndani ya tupu ya mwanamke lakini mwanamme hakutoa manii), na yeye alikuwa anajua kwamba hakuna kafara endapo hujatoa manii, lakini hajui kwamba kufanya jimai mchana wa Ramadhani ni haramu hata kama hukutoa manii?

**Jawabu:** ikiwa anaitakidi hivyo, basi funga yake ni sahihi, wala hakuna kulipa, kwa kauli ya Allaah: **"Ewe Mola wetu usituadhibu tukisahau au koukosea"**. **[Baqara/286].**

**Swali:** ikiwa (mtu amefanya) jimai (tendo la ndoa) zaidi ya mara moja kwa siku, au kwa mwezi mmoja, je, atatoa kafara zaidi ya moja vilevile?

**Jawabu:** iliyo mashuhuri katika madhehebu ya Ahmad Bin Hambal (Allaah amrehemu) ni kwamba: akiwa amefanya jimai zaidi ya mara moja kwa siku na akawa (alifanya mara ya pili n.k) kabla ya kulipa kafara ya mara ya kwanza, basi itamtosheleza yeye kafara moja tu.

Lakini akifanya katika siku tafauti (mfano alifanya katika siku ya kumi na siku ya kumi na tano katika mchana wa Ramadhani), basi atalipa kafara (mara mbili) kwa kila siku moja kafara yake, kwa sababu kila siku ina ibada yake inayojitegemea.

Markaz Sheikhil Islaam Ibn Taymiyyah

Pongwe Tanga

9/sha'ban/1444H – 2/3/2023H

Simu: 0715263253